



16 DAYS OF ACTIVISM AGAINST GENDER VIOLENCE
16 DÍAS DE ACTIVISMO CONTRA LA VIOLENCIA DE GÉNERO
16 JOURS D'ACTIVISME CONTRE LA VIOLENCE DE GENRE
25 NOV - 10 DEC <http://16dayscwg.rutgers.edu>



TAARIFA KARATASI # 1

Kuunganisha Haki za Wanawake, Haki za Binadamu Na Harakati za Amani kupunguza vita vya kimajeshi Na kumaliza Unyanyasaji dhidi ya Wanawake- Kwa miongo kadhaa, haki za wanawake, haki za binadamu na wanaharakati wa kutetea amani wamekuwa wakitetea matumizi ya mikakati ya amani kumaliza mgogoro na vurugu na kufikia haki za wanawake. Harakati hizi hupunguza miundo ya kijamii inayoruhusu ubaguzi kuendelea. Wakati sisi twaweza kuwa na mbinu mbalimbali ya kuleta duniani iliyo bora zaidi, utetezi katika maeneo haya ni asili kupunguza vita vya kimajeshi na kuweka mbele njia za jinsia za amani.

Nadharia za kike zinasisitiza haja ya mbinu shirikishi, ambao unahusu kuchunguza njia ambazo masuala kama vile usalama wa chakula, uharibifu wa mazingira, maslahi ya kampuni mbalimbali, haki za uzazi na ngono, umaskini, kutovumilia dini, ubaguzi wa rangi, nakadhalika, inahusika na vita vya kimajeshi. Kutambua uhusiano uliopo utaweza kuonyesha njia katika harakati mbalimbali ambayo yaweza kufaidi kutoka kwa shughuli hizi na kumaliza vita vya kimajeshi. Kutokana na mahusiano haya, na kuchochea mabadiliko ya kuleta mabadiliko ni muhimu kwamba haki za wanawake, haki za Binadamu na Harakati za amani kubadilishana taarifa. Vile vile, mazungumzo ya kimataifa ni muhimu kwa kuonyesha njia ambazo amani nyumbani zinao uhusiano na amani duniani.

Kwa watu wengi, hisia za salama hazitokani na silaha au jeshi. Badala yake, usalama ni juu ya uhuru wa kutembea, uhuru wa kujieleza, kuwa na kazi, chakula na upatikanaji wa maji safi, kuwa katika mahusiano ya upendo, na mengine mengi. mfumo wa haki za binadamu ambayo husisitiza hali halisi ya wanawake inaweza kusaidia kuwezesha malengo haya na kukuza ukweli kwamba amani ni muhimu kwa mafanikio ya maendeleo na usalama wa kweli..

Wakati wakuzungumzia miundo nguvu kubwa inayo kuza na kuendeleza unyanyasaji dhidi ya wanawake, wakati mwingine ni vigumu kujua wapi na jinsi ya kuanza. Kuuliza swali moja ni "Ni nani anayefaidika?" Migogoro ya mara kwa mara huhusiana na udhibiti wa rasimali ndani ya kile ambacho mara nyingi hujulikana kama tata ya kijeshi ya viwanda. Katika muktadha huu, uzalishaji na uuzaji wa silaha umeendelea kuwa sekta inayoongoza kimataifa. Kwa kuongeza, jeshi na makundi ya waasi mara nyingi hujihusisha na ukiukwaji wa haki za binadamu na kutumia rasilimali inayopata kwa njia ya vita kufadhili vita. Maswala yanayohusika ni pamoja na utetezi wa bajeti ya kitaifa, matumizi ya kijeshi, misaada ya kigeni na kijeshi, na Mashirika ya kimataifa yanayohusika kibinafsi na yasiyoshiriki kibinafsi katika maeneo ya vita.

Bila kujali 'kiingilio' unachochagua, tunatarajia utafikia washirika mpya katika harakati mbalimbali wakati wa kampeni wa mwaka huu. Kwa njia ya pamoja, tunaweza kuleta athari kubwa zaidi.

"Katika dunia ya kukosekana kwa utulivu na kuendelea na vurugu, utekelezaji wa mifumo ya vyama vya ushirika kwa amani na usalama vinatakiwa kwa haraka. fursa sawa na ushiriki wa wanawake katika miundo na nguvu na ushiriki wao kikamilifu katika juhudi zote kwa ajili ya kuzuia na kutatua migogoro ni muhimu kwa ajili ya matengenezo na kuimarisha amani na usalama "

-Beijing Platform for Action, E 134

"Sisi sote tulmealikwa kufanya kazi pamoja kwa amani. Tutaungana mikononi na akili ili tuweze kufanya kazi kwa amani kwa njia ya amani bila fujo. Tutasaidiana, tufarijiane na kujifunza kutoka kwa sisi wenyewe kwa wenyewe jinsi ya kuleta amani kwa watoto wetu na kila mtu kwa jumla

- Mairead Corrigan-Maguire, Ireland ya Kaskazini, 1976 Tuzo ya Amani ya Nobel

"Kila mtu ana haki ya uhuru wa maisha, na usalama wa mtu"

- Kifungu # 3, Universal Azimio la Haki za Binadamu

"Mimi ni mmoja tu, lakini bado mimi ni mmoja. Siwezi nikafanya kila kitu, lakini bado naweza nikafanya kitu fulani. Siwezi kukataa kufanya kitu naweza kufanya

- Helen Keller (1880-1968) mwanaharakati wa haki za wale mavu wa Marekani

Mapendekezo ya Hatua

- **Shawishi Serikali yako** Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limepitisha maazimio kadhaa (1325, 1820, 1888, 1889, na 1960) kuhusiana na wanawake, amani na usalama, na maserikali yakutakiwa kutekeleza ahadi hizo. Uliza serikali yako jinsi mipango ya hatua katika maazimio hayo, na ushawishi kuwepo kwa ushiriki wa wanawake katika kufanya maamuzi katika ngazi zote juu ya amani na masuala ya usalama, ikiwa ni pamoja na: mazungumzo ya amani; kusambaratisha; upunguzaji wa silaha; kuwarejeshea makwao; makazi mapya na kuwaunganisha na jamii; na fidia michakato na kujenga amani, ahueni na juhudi za ujenzi.
- **Unganisha Harakati:** Kuelekea kwenye siku 16 za kampeni, fikia nje kwa haki za wanawake, haki za binadamu, na mashirika ya amani ambayo hujawahi kufanya kazi nayo na uwaombe wakuunge kwa tukio fulani wakati wa kampeni. Kama inawezekana, fanya mikutano ya kupanga kabla ya muda ili uweze kujifunza zaidi juu ya kazi za kila mmoja na mitazamo yao.
- **Fuatilia matumizi ya Serikali:** Ligi ya Wanawake wa Kimataifa wa Amani na Uhuru (WILPF) imekuwa ikikusanya taarifa juu ya matumizi ya nchi za kijeshi na imeweka pamoja kiongozi cha kulinganisha matumizi ya kijeshi, ambayo imewekwa pamoja katika muundo huu wakuchukua hatua. Tumia miongozo yao ya utafiti kwa matumizi ya kijeshi ya nchi yako na utume matokeo ya uchunguzi wako kwa WILPF na CWGL!
- **Fuata Fedha:** Serikali siyo wale tu wanaohusika katika biashara ya vita. Tafuta makampuni ipi inayofaidika na migogoro au hutumia “madini ya migogoro” na uandike malalamiko au ugomeze bidhaa zao
- **Sherehekea:** Baada ya mifano chanya na kusikiliza hadithi ya mafanikio kuhusu harakati za wanawake wa amani ni muhimu kwa ajili ya ukuaji wa harakati zetu. Hutuhamisha kuendelea na harakati zetu katika nyakati ngumu na kutukumbusha ya kuwa sisi ni sehemu ya jitihada za nguvu ya kimataifa. Wakati wa Kampeni ya mwaka huu ya siku 16 kusherehekea mifano chanya katika maisha yako na kuelezana mifano ya wanawake wengine wanao fanya mabadiliko duniani kote. Waweza kutembelea [PeaceWomen Across the Globe](#) ili uweze kusoma kuhusu wanawake 1000 waliochaguliwa na kupewa nafasi kuweza kushinda Tuzo ya Nobel mwaka 2005 na ujifunze zaidi kuhusu kazi zao ujasiri na ubunifu kwa ajili ya amani na haki ya kijamii!
- **Usalama ni nini Kwako?:** Mwaka huu, CWGL inakuomba ushiriki katika mradi kwa ajili ya Kampeni ya kimataifa ya siku 16 ya kampeni ili kufafanua zaidi Usalama. Fanya Video ya sekunde 30, baadaye, itume kwa YouTube au popote kwenye Internet ambapo yaweza kuonyeshwa na kuwasilisha elekeza kwenye kiungo cha CWGL kwenye internet Pia unaweza kutuma kwetu taarifa fupi iliyoandikwa katika kiungo hicho. <http://16dayscwgl.rutgers.edu/2011-campaign/qwhat-is-securityq-submissions>.

Rasilimali

- Amnesty International: <http://www.amnesty.org/en/human-rights/human-rights-by-topic>
- AWID: Building Feminist Movements: <http://awid.org/Our-Initiatives/Building-Feminist-Movements-and-Organizations>
- FemLINK Pacific: www.femlinkpacific.org.fj
- Gender Action for Peace and Security: <http://www.gaps-uk.org/>
- Global Day of Action on Military Spending: <http://demilitarize.org>
- Global Network of Women Peacebuilders: <http://www.gnwp.org/>
- Human Rights Watch: <http://www.hrw.org/>
- International Peace Bureau: <http://ipb.org/i/index.html>
- NGO Working Group on Women, Peace and Security: <http://www.womenpeacesecurity.org/>
- WILPF. (2009) *You Get What you Pay For*. Available online from the Women's International League for Peace and Freedom: http://www.peacewomen.org/portal_resources_resource.php?id=528
- Women, War and Peace (UN Women): <http://www.womenwarpeace.org/>

Translated kindly by: Wanzala E. Martin, Allied Youth Initiative - Uganda

